



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



Unapojibu tafadhali taja:

NambayaZabuni: LGA/001/2022/2023/NC/01/L/1-5  
Kwa ajiliya: UWAKALA WA VYANZO VYA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA  
2022/2023

**MWALIKO/ TANGAZO LA ZABUNI**

Tarehe: 13/06/2022

1. Halmashauri ya Wilaya ya Meru inapenda kualika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa uwakala wa ukusanyaji wa mapato kutuma maombi yao kwa Zabuni hii.
2. Unaalikwa kuwasilisha Zabuni yako kwa ajili ya kukusanya Mapato ya usafi na Mazingira, mazao na madini ya ujenzi kama ilivyoainishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.
3. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Halmashauri ya Wilaya ya Meru kupitia TANEPS kabla ya tarehe 29/06/2022 saa tano na nusu asubuhi. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika kupitia TANEPS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilishwa Zabuni.
4. Waombaji wawe na vithibitisho vya kuwa na vifaa vya kazi kama magari/ Trekta kwa kusafirishia taka kwenda dambo, Vifaa vya kutosha vya kusafishia, wafanyakazi/vibarua wa kutosha kutokana na ukubwa wa eneo analoomba, pamoja na ofisi ya kudumu.
5. Baada ya kupata zabuni kampuni au Kikundi kiwe na Mabango makubwa ya rangi ya Kung'aa yatakayobandikwa katika magari ya kazi kwenye tela

upande wa kushoto na kulia na milango ya mbele yakiwa na ujumbe wa kuhamasisha usafi, namba za simu za viongozi wazabuni, sare za kazi za kutosha kwa wafanyakazi wote, Gum boot, Gloves ngumu za kutosha na reflector kwa wale watakaofanya usafi barabarani na ratiba za kazi kwa kila mtaa/kitongoji zipatikane kwa viongozi wa Kila mtaa/kitongoji.

6. Halmashauri ya Wilaya Meru haitatoa zabuni kwa Wakala yeyote anayedaiwa na Halmashauri au aliyewahi kupelekwa mahakamani kwa ajili ya madai mbalimbali ya kutowasilisha mapato kwa wakati.
7. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Aidha, mwombaji aliyewahi kushitakiana na Halmashauri ya Wilaya ya Meru kuhusiana na kazi yeyote, hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yeyote ya zabuni iliyotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Vile vile Waombaji watakaothibitika kuwa na tuhuma za utendaji usiozingatia Sheria kutoka Taasisi nyingine za Serikali hawatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi zinazotangazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Meru.
8. Mzabuni atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka dhamana ya BIMA (INSURANCE BOND) yenye thamani ya makusanyo ya miezi mitatu (3) kulingana na gharama ya mkataba wake. Dhamana hiyo itarudishwa baada ya mkataba kuisha, na endapo mzabuni atashindwa kutimiza masharti ya mkataba dhamana hiyo itatumika kutekeleza shughuli za sehemu ya mkataba mpaka atakapopatikana mzabuni mpya.
9. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti na TANePS au zilizowasilishwa katika muundo usio kubalika na TANePS, hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote.

**Mwl. Zainabu j. Makwinya** MKURUGEZI MTENDAJI  
Mkururugenzi Mtendaji (W) HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU  
S.L.P. 462 USA RIVER  
MERU - ARUSHA  
Halmashauri ya Wilaya ya Meru